# JARIDA LA ATD DUNIA YA NNE TANZANIA

Desemba 2017

"Popote pale wanaume kwa wanawake wanapolazimika kuishi katika maisha ya umaskini uliokithiri, haki za binadamu hukiukwa. Sote ni wajibu wetu wa dhati kujiunga pamoja na kuhakikisha kwamba haki hizi zinaheshimika". - Joseph Wresinski (1917-1988), founder of ATD Fourth World -



## Tahariri



Jarida hili ni hitimisho la mwaka mzima kwa harakati za ATD Dunia ya Nne. Miradi iliyowakutanisha watu, kutambua mapambano katika maisha yao ya kila siku, kwa watoto wao, familia zao. Maisha yao yanatukumbusha tena kwamba tunajukumu la kufahamu na kuwafanya watu kutambua nini maana ya kuishi kwa kuto tambuliwa na kuheshimiwa.

Utafiti wa kubaini viashiria vya umaskini bado unaendelea vizuri. Timu inafanya kazi na wawakilishi wa makundi katika jamii ya Dar es Salaam. Wanaume, wanawake, watoto, wazee, walemavu, wagonga mawe, wanataaluma n.k.

Tutashirikishana mambo tuliojifunza, mikutano, shuhuda zinatualika kwa pamoja kutafakari upya nini maana ya kuishi katika umaskini uliokithiri, umaskini uliokithiri sio tu kukosa pesa. Ni ukosefu wa amani, usalama wa kudumu. Mama mmoja mpishi katika soko la samaki ambae huibiwa vitu alivyonavyo wakati wowote ule au mama mwingine ambae anagonga mawe hana jinsi na humchukua mwane mdogo na kwenda nae machimbo ya kokoto na kumsaidia kazi. Mwaka 2018 tutakutana na watu wanaoishi kijijini.

Jarida hili pia ni maalum. Ni hitimisho la mradi wa Elimu Kwa Wote. Timu imeaandaa taarifa kutueleza taarifa tofauti kutoka katika mradi huu na kipi kilichofanikiwa. Mwaka huu 2017, mikutano ilivyoongeza uelewa na umoja baina ya walimu na wazazi kama ni njia moja ya mafanikio ambayo itawafanya watoto kuanza na kumaliza elimu yao ya msingi na kufikia malengo yao.

Pia tungependa kushirikishana nanyi katika siku muhimu ya mwaka, kwa kila mwaka, siku ya kutokomeza umaskini. Mamia ya wanaharakati hujumuika pamoja na kusema ni jukumu letu kuwa pamoja na wale wote wanaoishi katika hali ngumu na kufikia haki zao za msingi.

Nawatakia kheri ya mwaka mpya 2018 na nguvu na afya njema kwa kila mmoja kufikia melengo yetu ya kupambana na changamoto wanazokutana nazo watu wanaoishi katika umaskini.

Alexie Gasengayire
Mjumbe wa Timu ya Uongozi ya ATD

**"Mahusiano baina ya wazazi na sisi walimu yameimarika sana na wote huwa pamoja kwa kila jambo linalohusu shule". Mwalimu mkuu.**

Kwa kipindi cha mwaka mzima 2017 Timu ya elimu kwa wote ya ATD ilikuwa ikifanya kazi ya kusambaza matokeo ya utafiti mashuleni kwa kufanya mikutano ya wazi ambayo ilihudhuriwa na walimu, wazazi, viongozi wa serikali za mitaa, makatibu kata na madiwani ndani na nje ya Dar es Salaam.

Kwa lengo la kuongeza uelewa kati ya walimu, wazazi na wadau mbali mbali wa elimu kujadili na kulinda haki ya kila mtoto katika upatikanaji wa elimu ya msingi.

Timu ya Elimu kwa wote ilifanya mikutano 14 katika shule tofauti na kuwafikia idadi ya watu kwa ujumla walioshiriki mikutano yote ndani na nje ya Dar es Salaam ni 5,443.

Mikutano hii ilileta matokeo chanya katika jamii hususani mashuleni ambapo wazazi na walimu waliweza kuchangia na kuunda mikakati ya kuweza kuboresha maendeleo ya watoto katika upatikanaji wa elimu ya msingi kama tulivyoona mabadiliko hayo katika shule mbali mbali walimu wa kuu walitueleza juu ya mapendekezo yalivyoleta mabadiliko chanya katika shule zao na kujenga uhusiaono imara baina ya walimu, wazazi na viongozi wa serikali za mitaa kupitia mapendekezo 6, 11 na 14.

**Pendekezo 6**
**Wazazi wanapaswa kuwapatia watoto wao sare za shule, begi, viatu na kalamu. Wanapaswa kuwahamasisha watoto wao kusoma na kuwasikiliza hofu zao. Wazazi wawape watoto kazi za nyumbani zilizo ndani ya uwezo wao na zisizoingiliana na kazi zao za shule ya msingi.**

**Pendekezo 11**
**Kuwepo na mfumo wazi wa mawasiliano kati ya walimu na wazazi. Mawasiliano yanaweza kuwa kwa njia ya mikutano, simu, barua au kutembeleana.**

**Pendekezo 14**
**Mikutano ya shule iandaliwe na walimu wakuu na wawakilishi wa wazazi. Mikutano iwe ni sehemu ya wazazi na walimu kubadilishana uzoefu na changamoto wanazokutana nazo na kulenga zaidi maendeleo ya elimu ya watoto. Ni muhimu kwamba mawazo ya wazazi yasikilizwe.**

Maoni ya walimu wakuu……………

"Baada ya atd kufika shuleni na kufanya mkutano kumesaidia kuondosha matabaka, khofu na wazazi hufika shule kila mara na kufuatilia maendeleo ya watoto wao" mwalimu mkuu

"Wazazi wametambua majukumu yao ikiwemo kuwanunulia watoto wao sare za shule na vifaa vinavyohitajika na kuwafanya watoto kufika shule hali wakiwa wasafi na wenye kupendeza." mwalimu mkuu.

"Mahusiano baina ya wazazi na sisi walimu yameimarika sana na wote huwa pamoja kwa kila jambo linalohusu shule". Mwalimu mkuu.

"Wazazi hutembelea mara kwa mara shule na hukaa kwa pamoja na kujadili changamoto zinazotukabili na kufikiria njia ya kutatua changamoto hizo." Mwalimu mkuu.

Pia timu ya Elimu Kwa Wote iliweza kufanya mikutano na walimu wakuu,waratibu kata na maafisa elimu katika wilaya mbili ikiwemo wilaya ya Kinondoni ambayo idadi ya walimu wakuu walioshiriki katika mkutano huu wa kusambaza matokeo ya utafiti ni 60 na wilaya ya Ilala ambapo idadi ya watu waliohudhuria isiyopungua ni 260. Walimu wakuu na maafisa elimu walipokea kwa shauku mapendekezo yaliyopo ndani ya ripoti na kuweza kupatiwa nakala moja ya ripoti kamili kwa kila mmoja alieshiriki katika mkutano.

Kukamilisha zoezi hili la kusambaza matokeo ya utafiti katika kipindi hichi chote cha mwaka mzima timu ya elimu kwa wote inayoundwa na watu kutoka sekta mbali mbali walimu, mjumbe wa nyumba kumi, wanaharakati wa kujitolea wa kudumu wa ATD, wanafunzi na watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri. Kulikuwa na umuhimu mkubwa sana wa kuwepo na watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri katika timu hii ya elimu kwa wote.

Mama mmoja kutoka katika timu ya elimu kwa wote mwenye uzoefu wa kuishi katika umaskini uliokithiri kutoka Tegeta alitueleza umuhimu wake kushiriki katika mradi huu na umuhimu wa elimu kwa watoto wanaoishi katika umaskini uliokithiri. Alitueleza………

**"(…) kutokujua kusoma ni moja ya umaskini na ukijua kusoma unafunguka kiakili na unajua nini cha kufanya katika maisha yako na elimu ni njia ya kupambana na umaskini"**



Mei 2017
Mkutano shule ya msingi
Ikulu Mbeya
Rajabu, Bi Agnes, Shabani

“Nilifurahi sana kuwa mradi huu, maana hapo awali nilikuwa sijui kusoma wala kuandika lakini kupitia darasa la watu wazima ambalo linatolewa na ATD nilijifunza kusoma na kuandika. Kupitia elimu yangu hii ndogo nilioipata ukubwani iliniwezesha kushiriki katika mradi huu mkubwa unaohusu mambo ya elimu na nikiwa mwakilishi wa watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri kwa maana nami pia ni mmoja wa watu waoishi katika umaskini ilikuwa muhimu sana kusimama na kupaza sauti kwa kuyawakilisha Mapendekezo ambayo ni mawazo ya watu wanaoishi katika umaskini. Mapendekezo haya yalikuwa ni maneno muhimu sana kwani yalikuwa yakiiwaingia watu akilini na yalikuwa yana uhalisia katika maisha ya kila siku kwa watoto wanaosoma shule ya msingi. Pia lilikuwa ni jambo kubwa sana kwangu kwa maana sikuwahi kufikiria kulifanya maishani mwangu maana nilikuwa najua mambo ya utafiti na kuendesha mijadala mashuleni linafanywa na watu wasomi lakini kupitia mradi huu nimejifunza mambo mengi sana, kwani kutokujua kusoma ni moja ya umaskini na ukijua kusoma unafunguka kiakili na unajua nini cha kufanya katika maisha yako na elimu ni njia ya kupambana na umaskini”

Hii inatukumbusha katika kipindi cha utafiti mtoto mmoja alitueleza pia umuhimu wa elimu katika maisha ya kila siku, alisema:

“Elimu ni muhimu kwasababu kupitia hiyo naweza kufikia ndoto zangu, Elimu ni muhimu katika maisha yangu, mimi nikiwa mkubwa nitaweza kuwasaidia wazazi wangu. Elimu hutoa mwongozo katika maisha yetu ya baadae, Kama utakosa elimu inaweza kuwa sababu kubwa ya umaskini na Elimu hunisaidia kufikia malengo yangu. Elimu ni ukombozi wa maisha yangu, familia yangu na jamii yangu”.

Kuelekea mwaka 2018 timu ya Elimu Kwa Wote kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa elimu hapa nchi Tanzania itafanya semina shirikishi kutoa mrejesho juu ya mambo yaliopatikana katika kipindi cha kusambaza matokeo ya utafiti.



# Oktoba 17 mwezi oktoba siku ya kutokomeza umaskini uliokithiri Duniani. Maazimisho ya 30.

Atd Dunia ya Nne Tanzania ilianzimisha siku ya kutokomeza umaskini dunia, (maadhimisho ya miaka 30) siku ya Jumamosi tarehe 14 kabla ya sherehe za Oktoba 17 duniani kote kwa kila mwaka. Tukio hili lilifanyika Biafra sehemu ya wazi ili kuwawezesha wananchi wote kushiriki katika tukio hili. Kupitia maneno, maigizo, mziki na shuhuda tulionyesha jinsi umaskini uliokithiri unavyokandamiza uhuru wetu na kukiuka haki zetu za msingi. Shuhuda kutoka Dar es Salaam, Mbeya, Njombe na Dodoma zilitukumbusha mapambano dhidi ya umaskini na kutafuta njia ya amani. Oktoba 17 ilionyesha tena njia peke ya kuushinda umaskini uliokithiri na kupata amani na kuungana. Hii ni baadhi ya picha za matukio ya siku hiyo.















Wasiliana nasi!

ATD Dunia ya Nne - SLP 61786 - Dar es Salaam
Namba ya Ofisi: 0222761717
atd.tanzania@gmail.com
Kiswahili website: http://www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/tanzania/
Ukurasa wa Facebook: https://www.facebook.com/atd.duniayanne